OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA CHALINZE
SHULE YA SEKONDARI KIKARO. S L P 48, CHALINZE
KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA – 0789 021005 AU 0786 779039.

JANUARI 2021

Kumb: Na. KSS/A. 10/VOL III/ 13.

JINA MWANAFUNZI

……

…….

NDUGU

YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021</u>

Kichwa cha habari hapo juu cha husika:

Kwa barua hii nakujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika *Shule ya Sekondari Kikaro*. Natumia nafasi hii kukupongeza kupata nafasi hii adimu ambayo wengi wanaitamani na wameikosa. Bila shaka hutaipoteza "HONGERA SANA". Unatakiwa kufika shuleni ***tarehe 11 Januari 2021.***

Shule ya Sekondari Kikaro ipo mkoa wa Pwani wilaya ya Bagamoyo ndani ya **halmashauri ya Chalinze** katika kata ya Miono. Ukitoka Dar es salaam, panda magari yaendayo *Saadani au Miono* katika kituo cha daladala cha ***MBEZI YA KIMARA*** nauli ni Tsh **7000/=.** Ukitokea barabara ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga unatakiwa kushuka kituo cha **Mandera Kibaoni**, hapo utasubiria gari nyingine kwa nauli Tsh 1000/= na utafikishwa hadi shuleni. Ukitokea barabara ya Morogoro (hasa kwa wanaotokea mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Shinyanga n.k) utashukia kituo cham mabasi **CHALINZE** kisha utapanda gari nyingine zinazoelekea MIONO kwa nauli ya shilingi **4000/= tu**.

Pamoja na barua hii, naambatanisha fomu za maagizo maalum unayotakiwa kuyatimiza kabla ya kuja shuleni. Fomu hizo ni;

1. Fomu ya kukubali nafasi ya kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Kikaro
2. Fomu ya kupima Afya yako (iwe na muhuri wa Mganga Mkuu wa Mkoa/ Wilaya au Kituo cha Afya)
3. Fomu ya mwanafunzi atakaye pangishiwa chumba cha kuishi.

KUMBUKA: Fomu namba (1), (2) na (3) ukikamilisha kuzijaza uje nazo shule siku ya kuripoti.

Mkuu wa shule na wafanyakazi wengine wote wa shule hii wanakutarajia uwe mwanafunzi mtiifu, mwaminifu, nadhifu na mshiriki wa kazi zote za nje na ndani ya darasa.

ANGALIZO Hakikisha mwanao anakuja shuleni siku ya kufungua shule.

KARIBU SANA KIKARO SEKONDARI

……
EMMANUEL J. KAHABI

MKUU WA SHULE

FOMU NA. 01

HALMASHAURI YA CHALINZE

ANWANI YA MZAZI/MLEZI
S L P …….. .....

SIMU .....

E- mail……..……

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIKARO,
S L P 48,
CHALINZE.

YAH: UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021 SHULE YA SEKONDARI KIKARO.

SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI)

Mimi (jina kamili) …… niliyezaliwa tarehe ……Mwezi…… Mwaka …… Dini ……katika Kijiji cha …….. Wilaya ya …….. Mkoa wa……

Nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha kwanza *Shule ya Sekondari Kikaro*. Pia nitatii sheria na miongozo yote ya shule ambayo mwanafunzi anatakiwa kutekeleza na kutimiza.

SAHIHI YA MWANAFUNZI ……TAREHE …….

SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI)

Mimi ……. (Jina kamili) wa Kijiji cha …… kata ya …… wilaya ya ……Mkoa wa …… Kazi yangu ni …… namba yangu ya simu…….

Nafurahi sana kupokea nafasi aliyopewa mwanangu. Nitatekeleza na kutimiza maagizo yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na shule katika kumlea mtoto huyu kitaaluma, kinidhamu na kimaadili.

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI …… TAREHE ……..

SEHEMU C: (IJAZWE NA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI / KATA)

JINA…….. SAHIHI …….
TAREHE…….. MUHURI……

FOMU NA: 2

HALMASHAURI YA CHALINZE

SHULE YA SEKONDARI KIKARO
S.L.P. 48,
CHALINZE

TAREHE …….

YAH: KUPIMA AFYA (MEDICAL EXAMINATION)

Tafadhali mpime ……..

Kama afya yake inamruhusu kuendelea na masomo ya Sekondari kidato cha kwanza mwaka 2021

Andika NDIYO au HAPANA katika nafasi zilizoachwa wazi mbele ya ugonjwa kama aliugua.

1. Kifua Kikuu ……..
2. Ugonjwa wa moyo ……..
3. Ugonjwa wa figo ……..
4. Ugonjwa wa akili ……..
5. Ajali kubwa ……..
6. Pumu ……..
7. Vidonda vya tumbo ……..
8. Kifafa ……
9. Kupasuliwa ……
10. Mengineyo

……
……
……
……

MAELEZO YA MGANGA

……
……
……
……

JINA LA HOSPITALI /KITUO CHA AFYA ……..

JINA MGANGA:…… SAHIHI ……

TEREHE …… MUHURI ……

MAHITAJI YA SHULE

Yafuatayo ni mahitaji ya lazima unayotakiwa kuyatimiza kikamilifu. Ukumbuke kuripoti shuleni bila kukamilisha mahitaji haya, utakuwa umejinyima haki ya kusoma vizuri.

MAHITAJI KWA WOTE

i. Suruali nyeusi 02 zisiwe models upana wa chini usipungue 18''
ii. Mashati meupe mawili (02) mikono mifupi yasiyokuwa na urembo.
iii. Sketi 02 ndefu za kijivu yakukolea, kitambaa namba 01 (mshono wa linda box) ndefu ifike kwenye vifundo vya miguu.
iv. Viatu vya ngozi jozi mbili (02) rangi nyeusi (visiwe bajaji)
v. Sweta rangi dark blue zinaweza patikana mazingira ya shule
vi. Soksi jozi mbili rangi nyeusi kwa wavulana na rangi nyeupe kwa wasichana.
vii. Kwa wasichana wanaovaa hijabu shati ziwe za mikono mirefu zisizobana.
viii. Kila mwanafunzi ni lazima aje na fagio la chelewa lenye mti.

VIFAA VINGINE KWA WANAOISHI HOSTEL

i. Mchango wa chakula TSH 300,000.00 inayolipwa kwa awamu nne tu. Angalau Tsh. 75,000 kila awamu (**Januari 75,000/=, April 75,000/=, Julai 75,000/= na Septemba 75,000/=)**
ii. Shamba dress 2 za rangi ya dark blue kwa wanafunzi wa hostel (mshono wa solo)
iii. Shuka mbili (cotton) za blue bahari kwa wavulana na pink kwa wasichana zaweza patikana mazingira ya shule.
iv. Sanduku la bati la kuhifadhia vifaa vyake.
v. Chandarua rangi nyeupe, taulo na mto wa kulalia.
vi. Godoro moja futi mbili na nusu kwa sita (2.5x6x4'')
vii. Sahani, kijiko bakuli, kikombe na ndoo (02) zenye ujazo wa lita 10.
viii. Kwa wasichana waje na kanga doti mbili
ix. Vifaa vya michezo (**Jenzi ya taifa stars**, viatu vya michezo rangi nyeusi kwa wavulana na raba nyeupe kwa wasichana na soksi)
x. Aje na galoni ya lita tano (5) kwa ajili ya kuhifadhia maji yake ya kunywa mwenyewe.

Fedha zote ni lazima zilipwe Benki ya *NMB AKAUNTI Na:* ***21101100021.***
Jina : ***KIKARO SECONDARY SCHOOL****.*

NB:

- *MWANAFUNZI ANAYETAKA KUKAA HOSTEL ANATAKIWA KULIPIA GHARAMA ZA CHAKULA SI CHINI YA TSH 150,000.00 KWA MUHULA NA SI VINGINEVYO.*

- *MWANAFUNZI ANAYETAKA KUKAA HOSTEL AWE NA BIMA YA AFYA (* ***NHIF*** *au* ***BIMA ILIYOBORESHWA****) KWA ASIYEKUWA NAYO AWE TAYARI KUIPATA AKIWA SHULENI.*

SHERIA ZA SHULE

Katika jamii ni lazima kuwepo na sheria na kanuni ili kila mmoja aishi katika hali ya amani, usalama na utulivu. Aidha kuona kuwa kila mmoja anatendewa haki. Shule ya Sekondari Kikaro ni sehemu ya jamii hivyo inastahili kuwa na sheria za kuwaongoza na kuwalinda.

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule kama zilivyoanishwa kwenye mahitaji ya wanafunzi na si vinginevyo.
2. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shuleni na kufuata ratiba iliyowekwa
3. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtulivu na mkimya wakati wote anapokuwa darasani, mistalini na wakati wa kulala. Pia anatakiwa kuwepo darasani wakati wote kama hajaruhusiwa kutoka njee na kiongozi wa darasa au mwalimu.
4. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au mwanafunzi na mwalimu ni ya lugha ya kiingereza na si vinginevyo
5. Mwanafunzi anatakiwa kukaa shuleni wakati wote wa shule na ni marufuku kuvuka eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu wa zamu. Pia ;
    i. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutoka njee ya MIONO bila ya ruhusa ya MWALIMU WA MALEZI, MAKAMU MKUU WA SHULE NA MKUU WA SHULE
    ii. Wageni wote wafike ofisi ya malezi au matron kabla ya kuonana na mwanafunzi husika
    iii. Wanafunzi wa hostel watatembelewa jumapili ya mwisho wa mwezi tu
    iv. Wanafunzi wa hostel wataenda sokoni kila jumatano ya mwisho wa mwezi baada ya masomo.
6. Kila mwanafunzi anatakiwa kuonesha heshima ya hali ya juu kwa ;
    i. Kumsalimia kila mtu anayemzidi umri
    ii. Kumpokea mzigo mwalimu na aliyekuzidi umri.
    iii. Kutii bendera wa taifa kwa kusimama na kukaa mguu sawa inapopandishwa au kushushwa kwa mwongozo wa filimbi au mimbo wa taifa.
    iv. Kutii wimbo wa taifa unapoimbwa
    v. Kuwaheshimu viongozi wa serikali ya wanafunzi
    vi. Ni kosa kutoa kauli chafu au matusi, kupigana na kukashifiana na mwanafunzi mwenzio au mwalimu.
7. Kila mwanafunzi lazima awe nadhifu wakati wote ndani ya eneo la shule na nje ya shule. Ni marufuku kuvaa sketi fupi, nguo za kubana mwili, na ni kosa kuvaa kofia eneo la shule.
8. Ni jukumu la kila mwanafunzi kuhakikisha kuwa anatimiza wajibu wake kwa kushiriki kikamilifu katika kazi zote za elimu ya kujitegemea na utunzaji wa mzingira. Ni kosa kuharibu mazingira kwa kutupa karatasi ovyo, kuchoma moto na kukatiza kwenye viunga.
9. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa mwaminifu na mtunzaji wa mali za umma, pia ni kosa kusema uongo, kuiba na kuficha maovu.
10. Hairuhusiwi msichana kuingiza mvulana au mvulana kuingiza msichana bwenini.

11. Mwanafunzi bora sharti aoneshe tabia na mwenendo mzuri kwa kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viongozi , waalimu na wanafunzi wote. Hivyo hutakiwi kufanya yafuatayo;
    i. Kuingia na kutembea sehemu za starehe kama vilabu vya pombe/bar, maeneo ya disco nk.
    ii. Kufanya urafiki wa kimapenzi ukiwa mwanafunzi
    iii. Kutumia aina yeyote ya madawa ya kulevya. Kama vile bangi na kuvuta sigara.
    iv. Kunywa pombe na kulewa
    v. Kuzungumza na mwalimu au mtu anayekuzidi umri ukiwa umeweka mikono mfukoni au unatafuna kitu mdomoni
    vi. Kumiki simu ukiwa shuleni.
    vii. Kucheza kamali na michezo yote ya bahati na sibu ukiwa mwanafunzi.

KUMBUKA

Makosa yafuatayo yatamfanya mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja.knkl

i. Wizi
ii. Uasherati/ushoga
iii. Kuvuta bangi na kutumia madawa ya kulevya
iv. Kuharibu makusudi mali ya umma
v. Kupata kesi ya jinai kufuatana na sheria za nchi
vi. Kupigana na kumnyanyasa mwanafunzi, mwalimu au mtu yeyote
vii. Kudharau bendera ya taifa na kukosa utii kwa masuala ya kitaifa
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata au kusababisha mimba
x. Kutohudhuria masomo kwa muda siku tisini (90) mfululizo.

……

EMMANUEL J. KAHABI

MKUU WA SHULE

Fomu hii ijazwe endapo mwanafunzi atapangishiwa/geto chumba cha kuishi nje ya shule.

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

SHULE YA SEKONDARI KIKARO

MKATABA WA KUMPANGISHA MWANAFUNZI CHUMBA.

A: **IJAZWE NA MZAZI WA MWANAFUNZI:**

Mimi mzazi wa mwanafunzi ……. Wa kidato cha …….
Nimeamua kumpangia mwanangu chumba cha kuishi nikiwa na akili timamu kwa sababu.....
……
na nitahakikisha namtimizia mahitaji yake yote ya msingi kama mwanafunzi na kufuatilia nidhamu na taaluma yake. Endapo sitafanya hivyo hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.
Jina la mzazi……Sahihi ya mzazi…….....
Kijiji anachoishi ……. namba ya simu ya mzazi ……

B: IJAZWE NA BABA MWENYE NYUMBA (MPANGISHAJI):

Mimi ……mmiliki wa nyumba ambayo mwanafunzi …….. anaishi. Ninaahidi kusimamia nidhamu na mwenendo wa mwanafunzi na kutoa taarifa shuleni/ ofisi ya kijiji endapo tabia ya mwanafunzi mtajwa haitaridhisha.

Jina la Mpangishaji……Sahihi ya mpangishaji…….....

Kijiji ……kitongoji…….. namba yake ya simu……

C: IJAZWE NA MWANAFUNZI:

Mimi ……. Mwanafunzi wa shule ya sekondari Kikaro. Ninaahidi kuishi kwa kufuata kanuni na taratibu sahihi kipindi chote nitakachoishi katisha nyumba hii. Na endapo nitakiuka utaratibu adhabu kali ichukuliwe dhidi yangu.

SAHIHI ……. Tarehe ……

D: IJAZWE NA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHA MPANGISHAJI

Nathibitisha kuwa mwanafunzi ……..amepangiwa chumba katika kijiji changu. Na tutashirikiana kuhakikisha nidhamu ya mwanafunzi inakuwa bora.

SAHIHI……. Muhuri……. Tarehe ……..